# ATHARI ZA VALENSIA YA KITENZI KATIKA USARUFI WA MIUNDO YA KISWAHILI

*Mosol Kandagor*

*Chuo Kikuu cha Moi - Kenya*

*mosolkandagor@gmail.com*

*Salim Sawe*

*Chuo Kikuu cha Kabianga - Kenya*

*salimksawe@gmail.com*

## Ikisiri

*Wasemaji wa lugha huzingatia aina tatu za kanuni za uzuifu madhubuti zinazofungamana na valensia ya kitenzi katika uundaji wa sentensi za Kiswahili. Katika mkabala huo basi, makala hii inatambuai kwamba kanuni husika hubainika kwa sababu baadhi ya vijenzi (hasa nomino) vikiondolewa au vikiongezwa kwenye uambajengo wa kisintaksia, miundo isiyofasilika huzalishwa. Uchanganuzi unaofanywa katika makala hii unaonesha kwamba ufasili hauwezekani iwapo taarifa za kutosha hazitawakilishwa kwa wasikilizaji au ikiwa taarifa zisizofaa zitashirikishwa kwenye sentensi. Aidha, makala hii inaonesha kwamba kanuni tatu za uzuifu madhubuti ambazo ni za kanuni ya uzuifu wa valensia moja, kanuni ya uzuifu wa valensia mbili na kanuni ya uzuifu wa valensia tatu huhusu idadi ya nomino zinazohitajika kwenye muundo kwa mujibu wa kitenzi kilichotumiwa.*

**1.0 Utangulizi**

Kimsingi makala hii inahusu athari za valensia ya kitenzi katika tungo za lugha. Makala imejikita kwenye lugha ya Kiswahili ambapo watafiti wamedhihirisha kuwa wazungumzaji husika wa lugha huzingatia kanuni zanazodhibiti tungo. Uchanganuzi unaotolewa unaongozwa na Nadharia Amilifu Zalishi (NAZ) ambayo ni modeli inayolenga zaidi uchunguzi wa lugha kwa misingi ya Isimu Fafanuzi na Isimu Matini huku ikitilia maanani umuhimu wa vipengele vya kiisimujamii (Sawe, 2015; Sawe na Kipkosgei, 2017).

Nadharia Amilifu Zalishi iliendelezwa kwa kutilia maanani mseto wa mawazo ya Sarufi Zalishi, Isimu Amilifu, Umitindo, Isimu-Matini na hata Uchanganuzi Kilongo (Chomsky, 1965, 1993, 1995 & 2000; Halliday, 1985, Halliday na Matthiessen, 2004). NAZ inafafanua umilisi wa kiisimu kama ujuzi uliobwiwa akilini lakini inaeleza 'utendaji wa kiisimu' kama matumizi halisi ya lugha yanayoathiriwa na uamilifu, mitindo, uhusiano wa lugha, jamii na miktadha. Matokeo ya mifanyiko ya kiisimu inayofafanuliwa na NAZ hufanikisha mawasiliano (Kandagor na Sawe, 2019).

NAZ inafafanua kwamba kuna vipashio vinavyoungana kama satalaiti na nyuklia katika mchakato wa kuunda sentensi (Sawe na Mwamzandi, 2016; Kandagor na wenzake, 2017). Nyuklia ni kiini au kiambajengo kikuu cha muundo. Satalaiti nayo ni kitegemezi au kiambajengo chenye uamilifu wa kuijaliza nyuklia ya sentensi. Vitegemezi hutegemezwa kwenye viini kwa kulingana na sifa za kila kiini. Viini na vitegemezi vinavyojenga sentensi hujenga tao ambalo linaweza kuunganishwa na matao mengine ili kuunda kilongo.

Kwa mtazamo wa Nadharia Amilifu Zalishi, mofimu za kileksika na za kiuamilifu huteuliwa na kuunganishwa kwa kuzingatia mkuku na kanuni za kifonolojia, kimofolojia na za kisintaksia. Uteuzi na uunganishaji huo unaodhibitiwa na valensia hufanywa mara moja pasipo kuwa na nafasi ya kufanya mageuzi kinyume na ilivyodaiwa na Chomsky katika nadharia yake ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi (Chomsky, 1965; 1993).

Katika makala hii data ilikusanywa kwa kutumia mbinu ya sampuli ya kimakusudi kama inavyopendekezwa na Kombo na Tromp (2006). Kwa kurejelea methodolojia hii ya kukusanya data, watafiti walikusanya maneno, virai na sentensi kutokana na ujuzi wao katika matumizi ya lugha ya Kiswahili. Mbinu hiyo iliwawezesha kupata jumla ya tungo 22 ambazo ziliwasilishwa na kuhakikiwa katika makala hii. Aidha, miundo inayochanganuliwa katika makala hii ilikusanywa kutoka katika

mazungumzo ya wanafunzi na wahadhiri wa Chuo Kikuu kimoja nchini Kenya. Katika makala hii, usampulishaji lengwa ulitumika kuwateua watafitiwa watatu walioulizwa iwapo miundo iliyozalishwa kwa kuongeza au kupunguza vijenzi ilikuwa na maana. Mbinu hiyo ilitumiwa kisintaksia ili kuchunguza mchango wa valensia kwa usarufi wa sentensi. Utaratibu wa kuondoa baadhi ya viambajengo ulitufaa katika kubainisha kanuni zinazohusiana na valensia ya kitenzi.

Tukiongozwa na Nadharia Amilifu Zalishi, tulitumia watafitiwa watatu wenye umilisi wa Kiswahili ambao walikuwa wahadhiri wa Kiswahili ili kufanya maamuzi ya usarufi ya miundo iliyotumiwa kama mifano katika makala hii. Mintarafu ya Schutze na Sprouse (2013), maamuzi ya usarufi hutumika katika tafiti za kiisimu ili kuakisi kanuni za kiisimu zinazowakilishwa katika mfumo tambuzi. Maamuzi hayo ya usarufi huweza kufanywa na msemaji mmoja au zaidi wanaoteuliwa kwa kuzingatia umilisi wao (Schutze, 1996 na Myers, 2009). Miundo iliyothibitishwa kama isosarufi kuhusiana na mada imebainishwa kwa kinyota (*) katika makala hii.

## 2.0 Dhana ya Valensia ya Kitenzi

Valensia kwa mujibu wa Nadharia Amilifu Zalishi ni sifa ya kitenzi inayoukilia viambajengo vinavyoweza kushiriki katika ujenzi wa sentensi itakayozalishwa kwa kutumia kitenzi husika. Kwa hivyo, valensia inahusu sifa inayopatikana katika kila kitenzi inayodhibiti idadi ya nomino zinazoweza kushirikiana nacho ili kuunda sentensi (Sawe, 2015; Sawe na Kipkosgei, 2017). Kwa misingi hii, istilahi valensia inatumiwa kwa fahiwa tofauti katika NAZ na matumizi yake katika taaluma ya Kemia kwa maana ya idadi ya elektroni zinazopatikana kwenye kitegemezi cha elementi.

### 2.1 Kanuni za Uzuifu wa Valensia

Miundo inayochanganuliwa hapa chini inaonesha kuwa sifa au valensia ya kitenzi huamua iwapo yambwa itateuliwa kukifuata au la. Kitenzi kikuu huamua kiambajengo kitakachojitokeza kwenye shamirisho, kwa mfano, ikiwa ama nomino moja au mbili zitahitajika kimuundo baada ya kitenzi au hazihitajiki baada ya kitenzi husika. Kimsingi, vitenzi mahususi huamua idadi ya nomino zinazoweza kuunganishwa kama viambajengo vya sentensi. Aina zifuatazo za kanuni huzingatiwa katika sentensi za Kiswahili:

#### 2.1.1 Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Moja

Kanuni ya uzuifu wa valensia moja inahusiana na uzuifu madhubuti wa kisarufi na hutegemea uelekezi wa kitenzi katika ujenzi wa miundo ya kisintaksia. Kutozingatiwa kwa valensia ya kitenzi katika uundaji wa

sentensi kutasababisha kuzalishwa kwa muundo ambao haujakamilika kama sentensi au wenye vijenzi vingine visivyohitajika.

Kanuni ya uzuifu wa valensia moja inazingatiwa katika miundo yenye vitenzi visoelekezi. Kwa mujibu wa kanuni hii, kitenzi ambacho ni neno kuu katika KT$_{\mathbf{so}}$ hakiwezi kufuatwa moja kwa moja na KN. Virai vitenzi visoelekezi hutumiwa kujenga vishazi visoelekezi au sentensi zisoelekezi. Kirai kitenzi kisoelekezi huundwa kwa kuzingatia kanuni ya uzuifu wa valensia moja [**KUV$_1$ → [KN + T$_V^1$ + (KE)]]**. Kwa misingi hiyo, vishazi visoelekezi ni vile ambavyo vitenzi vyao vikuu si vielekezi. Muundo wa diskosi wenye vitenzi vikuu visoelekezi kwa hivyo utakosa muwala iwapo kitenzi chake kitajalizwa kwa KN kama inavyodhihirika katika mifano 1(c) na 1(b) inayofuata:

1 (a) Wazazi wamekuwa wakilalamika kwa sababu ya karo ambazo walimlipia
- lalamika
[ + KT [ __ ] [ - KN]]

(b) Wazazi wamekuwa wakilalamika'
- lalamika
[ + KT [ __ ] [ - KN]]

(c) *Wazazi wamekuwa wakilalamika <u>nyumba</u> kwa sababu ya karo ambazo walimlipia
- lalamika
*[ + KT [ __ ] [ + KN]]

2 (a) Yego anapenda kulala wakati tunaposafiri, hivyo inakuwa vigumu kusafiri naye kwa masafa marefu
- lala
[ + KT [ __ ] [ - KN]]

(b) *Yego anapenda kulala <u>kalamu</u> tunaposafiri.
- lala
*[ + KT [ __ ] [ + KN]]

Mifano hii ya vishazi visoelekezi inaashiria kwamba miundo yake inaweza kujitosheleza kisintaksia na kisemantiki kama sentensi pasi na kujalizwa kwa virai nomino katika nafasi ya yambwa. Vitenzi vikuu kama vile 'lalamika' na 'lala', haviwezi kufuatwa moja kwa moja na KN. Jaribio la kuunganisha KN baada ya vitenzi hivyo kama kijalizi huzalisha miundo isiyoeleweka na inayoathiri muwala wa kilongo kama 1 (b) na 2 (b) iliyokataliwa kabisa na wasailiwa. Baadhi ya vitenzi vya valensia moja ni vile vilivyoambikwa mofu za hali ya kutendeka au kuwezekana {-ik-}, {-ek-} au {-uk-} kama inavyodhihirishwa katika mifano (3) na (4) ifuatayo:

3 (a) Mlango mwingine umefunguka.

- funguka
[ + KT [ __ ] [ - KN]]

(b) *Mlango mwingine umefunguka <u>kitabu</u>
- funguka
*[ + KT [ __ ] [ + KN]]

4 (a) Shamba limelimika; anza kununua mbegu na mbolea.
- limika
[ + KT [ __ ] [ - KN]]

(b) * Shamba limelimika <u>ndizi</u>
- limika
*[ + KT [ __ ] [ + KN]]

Kukubalika mifano 3 (a) na 4 (a) na kukataliwa kwa mifano 3 (b) na 4 (b) kunathibitisha kwamba kanuni ya uzuifu wa valensia moja huzingatiwa katika uzalishaji wa sentensi.

Kanuni ya uzuifu wa valensia moja huruhusu kushirikishwa kwa chagizo pekee kama kijenzi cha hiari cha KT lakini hairuhusu kushirikishwa kwa KN kinachotekeleza dhima ya yambwa. Kutozingatiwa kwa kanuni hiyo husababisha uzalishaji wa usemi usiokuwa na muwala kama 5 (c). Vipashio vilivyopigiwa mstari katika mfano (5) vinachukuliwa kimuundo kuwa chagizo kwa vile usemi unaweza kudhihirisha muwala hata visiposhirikishwa katika sentensi. Hii inaashiria kuwa kisarufi, vipashio hivyo vinatekeleza uamilifu wa vielezi vinavyoweza kuondolewa pasipo kuibadilisha maana ya msingi ya KT. Usemi ufuatao wa M32B2 umerudiwa hapa kama mfano 5 a), (b) na (c):

5 (a) Wazazi wamekuwa wakilalamika kwa sababu ya pesa taslimu za karo walizomlipia tangu mwaka jana.

(b) Wazazi wamekuwa wakilalamika kwa sababu ya karo walizomlipia kwa pesa taslimu.

(c) Wazazi wamekuwa wakilalamika.

Mfano 5 (a) unaonesha kuwa vipashio vinavyoweza kuongezwa baada ya kitenzi kikuu cha kirai kitenzi kinachoundwa kwa kitenzi kikuu chenye valensia moja ili muwala wa usemi udumishwe ni pamoja na (i) virai elezi au chagizo na (ii) virai husishi. Chagizo ni sehemu inayoweza kuondolewa kwenye tungo bila kuparanganywa kwa maana. Chagizo huweza kuchangia mshikamano na muwala wa kilongo iwapo inarejelewa katika matao mbalimbali yanayojenga kilongo. Kuondolewa kwake katika hali kama hiyo kutaathiri muungano na muwala wa mazungumzo. Baadhi ya vishazi kama inavyodhihirika katika 5 (b), vilikuwa na chagizo (vielezi) kwenye

virai vitenzi. Mfano 5 (c) unathibitisha kwamba vitenzi visoelekezi vinaweza kujitokeza bila chagizo katika sentensi. Kwa kujikita katika kategoria ya virai vitenzi (KT), uhalisia huu ulidhihirisha kuwa katika sentensi za Kiswahili, kitenzi ambacho ni neno kuu la KT hudhibiti kiuambajengo vipengele vingine vinavyojitokeza ndani ya kirai hicho.

### 2.1.2 Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Mbili

Hii ni kanuni nyingine iliyozingatiwa na watafitiwa katika uzalishaji wa diskosi za Kiswahili. Kanuni ya uzuifu wa valensia mbili hufuatwa iwapo kitenzi ni kielekezi mosi na kinahitaji kujalizwa kwa nomino moja pekee. Kitenzi cha aina hiyo ni chenye valensia mbili kwa sababu ili kitumiwe katika sentensi, ni lazima nomino ya kiima na nomino ya yambwa zishirikishwe kwenye muundo. Mifano (6), (7) na (8) ifuatayo inabainisha kuwa kanuni ya uzuifu wa valensia mbili katika diskosi za kiwingi-lugha hutegemea sifa za kitenzi kilichoteuliwa. Kitenzi cha valensia mbili huzingatia kanuni **[$KUV_2$ $\rightarrow$ [KN + $T_V^2$ + KN]]**. Kwa mfano:

6. Mutua: Wanafunzi wameharibu.
   Mutahi: Nini?
   Mutua: Mpango wangu.

Kitenzi 'haribu' katika usemi wa Mutua kina valensia mbili. Matumizi yake katika usemi wa Kiswahili sanifu kama mfano (6) ni sharti yazingatie kanuni ya uzuifu wa valensia mbili ambayo ni **[$KUV_2$ $\rightarrow$ [KN + $T_V^2$ + KN]]**. Ingekuwa kwamba, mzungumzaji Mutua alikuwa akijua kile kilichoharibiwa, basi usemi wake wa kwanza ungeeleweka. Usemi wake haukueleweka kwa msikilizaji wake (Mutahi) kwa sababu hakuzingatia kanuni ya uzuifu wa valensia mbili kwa kutoshirikisha kijalizi cha kitenzi kielekezi 'haribu'. Hii inamaanisha kuwa msikilizaji (Mutahi) hakuwa akiibua uhusiano wa kimuwala, katika hali hiyo akataka kujua wameharibu 'nini?' Zamu mbili zilizochukuliwa na Mutua zimezalisha usemi "wanafunzi wameharibu mradi wangu" ambao unafasilika kwa sababu unadhihirisha uhusiano wa kimuwala na umetimiza hitaji la kanuni ya uzuifu wa valensia mbili kama inavyodhihirishwa katika mfano (7) ufuatao:

7 (a) Mutua: $^{[Zamu\ 1]}$(Wanafunzi wameharibu) + M5K5: $^{[Zamu\ 2]}$(mradi wangu).

$^{Wanafunzi}$ [KT[$T_V^{2\ wameharibu}$] [KN[N $^{mradi}$]][V $^{wangu}$].

Usemi wa Mutua ungekosa kufasilika iwapo sehemu ya pili haingezalishwa hasa kwa sababu msikilizaji hakuwa akijua kitendo kilichokuwa kikirejelewa na mzungumzaji, kama inavyooneshwa katika mfano 7 (b) ufuatao:

7 (b) *Wanafunzi wameharibu.

Mfano (8) ufuatao unaonesha kwamba valensia huhusishwa na sifa za kileksika za kitenzi kikuu kama kiambajengo cha lazima kinachoathiri uteuzi wa vijenzi vingine kama vile nomino ya kiima na yambwa katika ujenzi wa diskosi. Hii ni kwa vile kitenzi ‘gonga’, kwa mujibu wa valensia yake, kinahitaji muundo unaohusika ushirikishe dhima mbili za uhusika wa kisarufi. Yaani, matumizi ya kitenzi hiki hufuata kanuni inayoelekeza ulazima wa kushirikishwa kwa nomino za mtenda na mtendwa katika muundo wa kilongo kama vile inavyofanyika katika mfano ufuatao:

8 (a) Ilikuwaje na uso wako? Jiwe lilinigonga nyumbani.

Muwala umeibuliwa baina ya usemi wa mzungumzaji na msikilizaji kwa sababu zamu ya kwanza inajenga kiini cha tao **[swali]** huku zamu ya pili ikijenga kitegemezi chake **[jibu]**. Kimantiki muundo 8 (a) unafasilika kama [S[KN[N$^{Jiwe}$[KT[T$^{lili\square ni\square gonga}$][KN[W$^{(Ø\ \square)}$][KE [E$^{nyumbani}$]]]]. Hii ni kwa vile kitenzi kielekezi mosi ‘gonga’ kimejalizwa kwa kiwakilishi cha nomino ‘ni’. Kwa hivyo, muundo 8(a) una muwala na umezingatia kanuni ya uzuifu wa valensia mbili [$\mathbf{KUV_2 \rightarrow [KN + T_V{}^2 + KN]]}$. Uhusiano kati ya muwala na valensia unadhihirika katika mfano huo kwa sababu aliyerejelewa kwa kimilikishi ‘wako’ ni msikilizaji anayechukua zamu na kujirejelea kwa kiwakilishi cha nafsi ‘ni’. Mfano 8 (b) ufuatao unadhihirisha kwamba kutozingatiwa kwa kanuni ya uzuifu kutazalisha miundo isiyobeba maana na kutaathiri mtiririko au muwala wa diskosi:

8 (b) *Jiwe liligonga nyumbani.

Mfano 8 (b) haujazingatia kanuni ya uzuifu wa valensia mbili kwa vile hauna yambwa tendwa (mtendwa au kitendwa) inayohusishwa na kitenzi ‘gonga’ na kwa hivyo haujitoshelezi kimuundo. Msikilizaji wa muundo kama 8 (b) atachanganyikiwa na kushindwa kuibua muwala kwa maana atashindwa kubaini nomino ipi iligongwa na jiwe. Hali hiyo itaibuka kwa sababu taarifa zinazohusu kiima katika kiarifu hazijashirikishwa.

Vitenzi vya valensia mbili ‘taka’ na ‘penda’ vinavyojitokeza katika mifano (9), (10) na (11) vimejalizwa kwa nomino za vitenzi-jina. Mintarafu ya msambao wa kategoria za kileksika katika diskosi zenye U.M., vitenzi vyenyewe visoukomo ambavyo ni vielekezi mosi viliweza kujalizwa kwa vitenzi jina katika mazungumzo ya watafitiwa kama ifuatavyo:

9. Mutahi anapenda kuwaza sana kuhusu mambo yasiyowezekana.
[KT$^{anapenda}$ ][KN$^{kuwaza\ sana\ kuhusu\ mambo\ yasiyowezekana}$]

10. Askari wanataka kushiriki katika hiyo warsha.
[KT$^{wanataka}$][KN $^{kushiriki}$]

11. Wasimamizi hawapendi wizi wa kiakademia.
[KT$^{hawapendi}$ ][KN $^{wizi\ wa\ kiakademia}$]

Mofu 'penda' na 'taka' ni vitenzi vya valensia mbili vinavyohitaji kujalizwa kwa virai nomino. Kanuni ya udhibiti wa valensia mbili ni sehemu ya umilisi wa wanawingi-lugha wanaojua vitenzi vyenyewe. Hii inamaanisha kuwa ujuzi wa vitenzi hivi huambatana na ujuzi wa kanuni hiyo inayomhitaji mzungumzaji avijalize kwa KN wakati wowote anavyovitumia. Kwa vile msikilizaji ana umilisi huohuo wa kanuni zinazohusu vitenzi vielekezi hivyo, kule kutozingatiwa kutasababisha ukosefu wa mantiki au muwala katika mazungumzo. Vitenzi vya sentensi (9), (10) na (11) kwa hivyo, vimejalizwa kwa usahihi kwa matumizi ya virai nomino vinavyoundwa kwa nomino za aina mbalimbali, kama vile 'kuwaza', 'kushiriki' na 'wizi wa kiakademia.'

Mifano (9), (10) na (11) inaonesha pia kwamba, vishazi vielekezi mosi huundwa kwa vitenzi vielekezi vyenye valensia mbili. Hata hivyo, kuna miundo ambayo ingawa ilikuwa na vitenzi vya valensia tatu, haikujalizwa kwa virai nomino. Katika hali kama hiyo, kirai nomino ambacho kingejaliza kitenzi husika hudondoshwa kwa sababu kilikuwa kimetajwa hapo kabla au kinafahamika kwa wale wanaosikiliza. Mfanyiko huo hujitokeza kwa vile viima na yambwa vinaweza kudondoshwa katika Kiswahili. Utafiti huu uligundua kwa mujibu wa mifano (12)-(14) kwamba udondoshaji hufanyika iwapo tu msikilizaji anatarajiwa kugundua ni faridi ipi iliyodondoshwa iwapo faridi hiyo itashiriki katika uwakilishaji wa maana. Ilibainika katika uchunguzi huu kuwa udondoshaji huambatana na matumizi ya kiwakilishi kitakachowakilisha nomino itakayodondoshwa ikiwa kitenzi kilichotumiwa kilikuwa kielekezi mosi.

Baadhi ya vishazi vielekezi vinavyojengwa kwa vitenzi vyenye valensia mbili havioneshi ama kirai nomino kimoja au vyote viwili katika kifundo cha kiima au cha yambwa katika umbo la kifonetiki lakini vipashio hivyo hujitokeza katika umbo la kimantiki. Kuwapo kwa viambajengo hivyo vya lazima kwenye umbo la kimantiki kunavifanya vishazi husika kukubalika kisarufi na kuchangia muwala wa diskosi. Mifano (12), (13) na (14) ifuatayo iliyozalishwa na watafitiwa kutoka bewa la kwanza na la pili inaweka wazi utendakazi wa kanuni ya uzuifu madhubuti ambao ni wa valensia mbili:

12 (a) Wakili aliyejitambulisha alitufanyia kadirio la thamani jana.
(b) *Alitanguliza.

13 (a) Lango lilijifunga.
(b) *Lilijifunga.

14 (a) Mtawaarifu.
(b) *Mliarifu.

Kama inavyobainishwa katika Jedwali 5.1, mifano (12) na (13) inaashiria kwamba kirai nomino cha kiima au kirai nomino cha yambwa kisichojitokeza moja kwa moja katika umbo la kifonetiki huwakilishwa na kiambishi kipatanishi cha kiima ($Kpt^K$) na kiambishi kipatanishi cha yambwa ($Kpt^Y$). Aidha, Jedwali linabainisha kuwa vijenzi hivyo visivyojitokeza moja kwa moja katika umbo la kifonetiki hujitokeza katika umbo la kimantiki.

**Jedwali 1: Uwakilishaji wa Vijirejeshi katika Umbo la Mantiki**

| | **Umbo la Kifonetiki (π)** | **→** | **Umbo la Kimantiki (λ)** |
|---|---|---|---|
| 12. | Alijitanguliza. | → | (Wakili) -tanguliza (wakili). |
| 13. | Lilijifunga. | → | (Lango) -funga (lango). |

Ili kujenga diskosi yenye mshikamano au inayofasilika, kanuni ya uelekezi na kanuni ya ujirejeleaji huzingatiwa katika kukipachika kiambishi kijirejeshi '-ji-' baada ya viambishi awali na kabla ya mzizi wa kitenzi. Kiambishi hiki kinaunganisha kitenzi kwa kiima na yambwa katika akili ya msikilizaji. Uziada ambao ungesababishwa na kurudiwa kwa nomino au kiwakilishi chake unaoondolewa kwa kutumia mofu ya ujirejeshaji '-ji-.' Mifano (12) na (13) inaashiria kwamba, matumizi ya mofu hii huweza kusababisha kudondoshwa kwa baadhi ya viambajengo kama vile nomino ya yambwa au ya kiima au zote mbili.

Vitenzi viwili [tanguliza] na [arifu] ni vielekezi kwa misingi kwamba visipofuatwa na KN, kanuni ya uelekezi mosi haitakuwa imezingatiwa. Jambo hili huzua maswali kama vile 'alitanguliza 'nani' au 'nini?' kama katika 12 (b) na arifu 'nani?' kama katika 14 (b) huibuliwa na miundo ya aina hiyo. Kuibuliwa kwa maswali haya kunamaanisha muundo si sahihi na hauwezi kuchangia muwala wa diskosi. Miundo yoyote – kama mifano kinzani 12 (b), 13 (b) na 14 (b) inayokaidi kanuni ya uzuifu wa valensia mbili $[\mathbf{KUV_2} \rightarrow [\mathbf{KN + T_V^2 + KN + (E)}]]$ isiyoeleweka (iso-sarufi).

Kanuni ya uzuifu wa valensia moja $[\mathbf{KUV_2} \rightarrow [\mathbf{KN + T_V^2 + KN + (E)}]]$ ilizingatiwa katika vishazi 12 (a) na 14 (a) kwa vile nomino ya yambwa zimebainishwa kwenye umbo la kifonetiki kwa kiambishi -{ji}- katika 'Alijitanguliza' na kwa kiambishi -{wa}- katika 'Mtawaarifu'. Kutokana na ruwaza za kimuundo zilizobainika katika sehemu hii, inaonekana kuwa vitenzi vyenye valensia mbili katika diskosi zenye U.M. hufuatwa na kirai

nomino kimoja tu kinachoweza kuwakilishwa kwa kiambishi kipatanishi cha yambwa.

Miundo hii miwili, '*Alitutanguliza'* na '*Mtawaarifu'* na mifano yao kinzani ni ithibati mwafaka kwamba uwakilishaji (wala sio udondoshaji) kama unaodhihirika katika mifano (12), (13) na (14) kwa viambishi '-ji-' na '-wa-' huchangia mshikamano baina ya vipande vya diskosi zenye U.M. Virai nomino vinavyodondoshwa ni vile vyenye sifa hafifu vinavyodhihirika tu katika Umbo la Kimantiki (λ) lakini zisizodhihirika katika Umbo la Kifonetiki. Nomino zenye sifa imara hazidondoshwi na kwa hivyo hujitokeza katika Umbo la Kifonetiki (π). Kipashio kilichodondoshwa katika mfano 12 (a) ni KN ambacho kingerudiwa kama yambwa 'wakili' na kile kilichodondoshwa katika 13 (a) ni KN cha yambwa pia 'simu'. Kwa vile viungo vya mshikamano hudhihirika kwenye umbo la kifonetiki, udondoshaji ambao unafanyika katika umbo la kimantiki hauwezi kuwa kiungo cha mshikamano.

Imebainika katika baadhi ya miundo kama (15), (16) na (17) kuwa vishazi vielekezi vinavyojengwa kwa KT chenye kitenzi cha valensia mbili (au ni kielekezi mosi) vinaweza kuzalishwa kwa sababu kitenzi kipo katika hali ya utendwa. Sifa za uelekezi wa kitenzi hudumishwa hata kama sentensi ni tendwa na ni lazima kitenzi kielekezi kishamirishwe kwa idadi sahihi ya nomino hata kama mtenda ($N_1$) atajitokeza baada ya mtendewa ($N_2$). Kutozingatiwa kwa kanuni ya uzuifu wa valensia mbili katika sentensi tendi (*active sentence*) au sentensi tendwa (*passive sentence*) kunaweza kuzalisha miundo isiyokuwa na maana au mantiki kwa jinsi itakavyoathiri muwala wa diskosi nzima. Miundo (15), (16) na (17) ifuatayo ni mifano ya sentensi tendwa zinazozingatia kanuni ya uzuifu wa valensia moja:

15 (a) Distribyuta ziliharibiwa na kiwango kilichokithiri cha umeme.
(b) Kiwango kilichokithiri cha umeme kiliharibu distribyuta.

16 (a) Fundi huyo aliniharibia diski ngumu yangu.
(b) Diski ngumu yangu iliharibiwa na huyo fundi.

17 (a) Mfadhaiko ulimwathiri mwalimu.
(b) Mwalimu aliathiriwa na mfadhaiko.

Makala hii inafafanua kwa mujibu wa Nadharia Amilifu Zalishi kwamba, wazungumzaji huzalisha diskosi zenye U.M. jinsi zinavyotamkwa. Sentensi hazifanyiwi mageuzi yoyote ya kimofolojia kama ya utendwi kama inavyofafanuliwa katika Nadharia ya Sarufi-Geuza-Maumbo-Zalishi (Chomsky, 1965). Dai kwamba kuna mageuzi ya kisarufi katika uzalishaji wa diskosi, kwa hivyo, si sahihi. Vile tulivyokwishakueleza hapo juu, kwa

mtazamo wa Nadharia Amilifu Zalishi, mofimu za kileksika na za kiuamilifu huteuliwa na kuunganishwa kwa kuzingatia mkuku na kanuni za kifonolojia, kimofolojia na za kisintaksia. Uteuzi na uunganishaji huo wenye uzuifu huongozwa na valensia na sifa nyinginezo za msamiati hufanywa mara moja pasipo nafasi ya kufanya mageuzi.

### 2.1.3 Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Tatu

Miundo yenye U.M. iliyokusanywa kutoka kwa mazungumzo ya watafitiwa iliyokuwa na vitenzi vyenye sifa ya uelekezi maradufu vilikuwa vikizingatia kanuni ya uzuifu wa valensia tatu [$\mathbf{KUV_3 \rightarrow [KN + T_V^3 + KN_1 + (KH) + KN_2]}$] kwa kushirikisha nomino mbili kwenye KT na nomino moja au kiwakilishi chake kabla ya kitenzi. Inabainika katika sehemu hii pia kwamba kupuuzwa kwa kanuni hii huathiri ujenzi wa mazungumzo yenye muwala.

Kitenzi kielekezi mosi ‘nunua’ kilichoteuliwa na mzungumzaji M10B1 katika Diskosi (18) kina valensia mbili lakini kuongezwa mofu (kitendea ‘i’ na kiishio ‘a’) za Kiswahili kukageuza kuwa kitenzi kielekezi maradufu chenye valensia tatu (nunulia). Diskosi 162 (a) iliyozalishwa na mtafitiwa kwa hivyo ni sahihi kwa sababu inazingatia kanuni ya uzuifu wa valensia tatu. Kutumiwa kwa kiunganishi ‘au’ katika diskosi hii kumechangia kuleta mshikamano baina ya vishazi viwili vilivyounganishwa. Vipashio ambavyo vingesababisha uziada kama ‘wewe’ na ‘sisi’ katika mfano huo (18 (a)) vilidondoshwa.
Miundo 18 (b) na 19 (c) iliyozalishwa na mtafiti kutokana na 18 (a) haizingatii kanuni ya uzuifu wa valensia tatu. Mifano 18 (b) na (c)) si sahihi kisarufi na haina muwala kwa sababu msikilizaji anatarajia kubainisha uhusiano wa kimuwala baina ya kiini ‘utatununulia’ na kitegemezi chake ambacho hakijatajwa. Kwa sababu ya kukosa muwala, msikilizaji katika mfano 18 (b) aliuliza “nunulia ‘nini’?” Kwa sababu muundo huo unaojengwa kwa kitenzi chenye valensia tatu una nomino moja inayowakilishwa kwa kiambishi ‘-tu-’ kwenye KT lakini hauna nomino nyingine inayohitajika. Msikilizaji huyohuyo aliweza kuuliza maswali mawili ‘nunulia nani nini?’ kuhusiana na 18 (c). Hii ni kwa vile mfano huo hauna nomino hata moja kwenye KT ilhali nomino mbili zilihitajika kama viambajengo vyake. Kwa mfano:

18 (a) Utatununulia chamcha au soda?
$KN_1[W^{(Wewe)}]][KT[T^{utatununulia}][KN_2[W_2^{(sisi)}][N^{chamcha}]]]$ au $[KN_3[W_3^{(wewe)}]][KT_2[T_2^{utatununulia}]$ $[KN_4[W_4^{sisi}][N_2^{soda}]$

18 (b) *Utatununulia?
18 (c) *Utanunulia?

Vitenzi vya valensia tatu ambavyo vinashurutisha kuzingatiwa kwa kanuni ya uzuifu valensia tatu katika miundo (19) na (20) ni vile vinavyohusu kufanya kwa niaba ya au hali ya kutendea. Kwa vile vitenzi vyenyewe vinadhihirisha uelekezi maradufu, vitaibua ulazima wa kuwapo kwa nomino itakayobainisha 'mtendewa' au 'kitendewa' wakati wowote vitatumiwa. Mifano (19) na (20) ifuatayo inaonesha kuzingatiwa kwa kanuni ya uzuifu wa valensia tatu.

19. Nilimwandikia Juma arafa lakini hakujibu.

$[S[KN[W^{ø}][KT[T_{V}{}^{3\ Nilimwandikia}][KN2[N2^{\ mzee}]]\ [KN3[N3^{\ ujumbe}]\ [---]]]$

20. Mudiri aliweka ofisi yake mapazia mapya.

$[S[KN[N^{Mudiri}][KT[T_{V}{}^{3\ aliweka}][KN_2[N_2{}^{ofisi}][KV[V^{yake}][KN_3{}^{mapazia}]\ [V^{mapya}]]]].$

Kupuuzwa kwa kanuni ya uzuifu wa valensia tatu huzalisha miundo ya Kiswahili isiyokuwa sahihi. Mifano 21 (a) na 22 (a) ifuatayo iliyozalishwa katika bewa la pili na mifano 21(b) na (c) pamoja na 22 (b) na (c) iliyozalishwa kwa kuondoa viambajengo vingine inaashiria kuwa kanuni ya uzuifu wa valensia tatu inazingatiwa katika sentensi za Kiswahili. Kwa mfano:

21 (a) Profesa hajawaidhinishia wale wageni vyeti.

$[S[KN[N^{Profesa}][[KT[T^{hajawaidhinishia}][KN2[V^{\ wale}]\ ][N_2{}^{wageni}]]][KN_3[N_3{}^{vyeti}]].$

(b) *Profesa hajawaidhinishia wale wageni.

(c) *Profesa hajaidhinishia vyeti.

22 (a) M23B2: Daktari anamwinulia Mungu mikono akiabudu.

$[S[KN[N^{(Daktari)}]][KT[T^{anamwinulia}][KN_2[N_2{}^{Mungu}][KN_3[N_3{}^{mikono}]][KT_2[T_3{}^{akiabudu}].$

'Daktari alimwinulia Mungu mikono akimwabudu'.

(b) *Daktari anammwinulia Mungu akimwabudu.

(c) *Daktari anamwinulia mikono akiabudu.

Nomino ya kwanza katika mifano 21 (a) na 22 (a) ni yambwa tendewa na ya pili ni yambwa tendwa. Uteuzi wa vitenzi na nomino kutoka lugha

mbalimbali ni sehemu ya uhuru wa mzumgumzaji unaofungamana na umilisi wake wa lugha.

Uambishaji wa kinyambulishi cha uhusika ala au cha kutendea katika Kiswahili {-i-} au alomofu yake {-e-} baada ya mizizi ya Kiingereza kama vile ‘nunulia’ na ‘idhinishia’, ‘andikia’, ‘wekea’ na ‘nunulia’ kama inavyoonekana katika (21) na (22) hubadilisha sifa za kisarufi na kuvifanya vipashio hivyo kuwa vitenzi vielekezi maradufu vyenye valensia tatu katika sentensi.


Kwa ujumla, uchanganuzi huu umedhihirisha kwamba masharti zuizi huzingatiwa katika uzalishaji wa sentensi. Ili muwala uendelezwe katika mazungumzo sehemu hii imeonesha kuwa: [i] vitenzi vya valensia mbili vikitumiwa katika kishazi, ni sharti vitanguliwe na nomino moja na vifuatwe na nomino moja au viwakilishi vyake; [ii] vitenzi vya valensia mbili navyo ni lazima vitanguliwe na nomino moja kisha vifuatwe na nomino mbili au viwakilishi vyake na hatimaye [iii] vitenzi vyenye valensia moja hutanguliwa na nomino moja au kiwakilishi lakini havifuatwi na nomino yoyote. Hali hii inaakisi kwamba ujuzi wa masharti zuizi ni sehemu ya umilisi uliobwiwa na watumiaji wa lugha.

Aidha, miundo iliyochanganuliwa hapo juu inaonesha kuwa kanuni hizo za uzuifu wa valensia moja, mbili au tatu zinahusu sifa za kitenzi kinachotumiwa kwa ujenzi sentensi na wala hazihusu sentensi kwa ujumla. Valensi ni elementi inayofungamana na faridi moja moja ya kileksika.
Isitoshe, uchanganuzi wa data uliofanywa hapo juu umeonesha kwamba kuna kanuni za uzuifu madhubuti zinazozingatiwa na wasemaji ili diskosi zao ziweze kuwa na muwala. Kanuni hizo zinazodhibiti ujenzi wa KT zinahusu idadi ya nomino zinazoweza kuwa viambajengo vya KT na huweza kubainishwa kwa muhtasari kama ifuatavyo:

**Kanuni za uzuifu madhubuti:**


(a) Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Moja

**$KUV_1 = KN + T_V^1 + (KE)$**





(b) Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Mbili

**$KUV_2 = KN + T_V^2 + KN + (KE)$**




(c) Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Tatu

**$KUV_3 = KN_1 + T_V^3 + KN_2 + (KH) + KN_3 + (KE)$**




Inabainika pia katika sehemu hii kwamba, kitenzi cha valensia moja ($T_V^1$) katika muundo hakiwezi kufuatwa moja kwa moja na KN. Kitenzi cha valensia tatu ($T_V^2$) nacho ni sharti kifuatwe na virai nomino viwili, vinginevyo KT kitakachoundwa na hata muundo utakaozalishwa hautapitisha maana kamili.

**3.0 Hitimisho**

Kwa kuongozwa na NAZ, makala hii inahitimisha kuwa uzalishwaji wa sentensi hufanywa pasipo urejelezi wa kufanya mageuzi yoyote ya baadaye kama ya utendwi au ya kimofolojia yaliyodaiwa na Nadharia ya Sarufi-Geuza-Maumbo-Zalishi. Aidha, makala hii inaonesha kwamba vipashio ambavyo havijanasuliwa akilini kutoka mwanzo kama vile mofimu za kileksika na za kiuamilifu huteuliwa na kuunganishwa kwa kuzingatia mkuku na kanuni za kifonolojia, kimofolojia na za kisintaksia. Uteuzi na uunganishaji huo wenye uzuifu unaoongozwa na valensia na sifa nyinginezo za msamiati hufanywa mara moja pasipo nafasi ya kufanya mageuzi. Uamuzi wa elementi nyingine zinazochaguliwa kwa ajili ya kujenga sentensi huathiriwa na masuala ya kijamii.

**Marejeleo**

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. Cambridge, Massachusetts: MIT Press.

Chomsky, N. (1993). “A Minimalist Program for Linguistic Theory” Katika K. Hale na S. Jay (Wah.). *The View from Building 20: Essays in Honor of Sylvain Brombeger.* Cambridge, Massachusetts: MIT Press.

Chomsky, N. (1995). *The Minimalist Program*. Cambridge: MIT Press.

Chomsky, N. (2000). *New Horizons in the Study of Language and the Mind*. Massachusetts: MIT Press.

Halliday, M. (1985). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Edward Arnold.

Halliday, M. & Matthiessen, M. (2004). *An Introduction to Functional Grammar*. London: Arnold Publishers.

Kandagor, M. na Sawe, S. (2019). Muwala katika diskosi za wingi-lugha. *JAKIIKI. 1*, 80-90.

Kandagor, M., Wendo, N. na Sawe, S. (2017). Role of indegenous languages in the development of county Governments. *Kioo cha Lugha*. 15, 65-74.

Kombo, K. D. na Tromp, L. A. D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Pauline Publications Africa.

Myers, J. (2009). Syntactic judgment experiments. *Language & Linguistics Compass*. 3, 406–423.

Sawe, S. (2015). Mshikamano na Muwala katika Diskosi za Kiwingi-lugha: Hali katika Vyuo Vikuu Nchini Kenya. Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Laikipia.

Sawe, S. na Kipkosgei, A. (2017). A Case of unmarked register in mathematical linguistics. *Ellixir*. 12, 26-30.

Sawe, S. na Mwamzandi, I. (2016). Logic as a semantic resource in the language of law and religion. *International Journal of Multidisciplinary Research Review*. 12, 45-48.

Schutze, T. (1996). *The Emperical Base of Linguistics: Grammaticality Judgements and Linguistic Methodology*. Chicago: University of Chicago Press.

Schutze, T. na Sprouse, J. (2013). *Reseach Methods in Linguistics.* Cambridge: Cambridge University Press.

Wasow, T. na Arnold, J. (2005). Intuitions in linguistic argumentation. *Lingua*. 115, 1481–1496.

**Alama na Vifupisho Vilivyotumika**

$KUV_1$ = Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Moja
$KUV_2$ = Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Moja
$KUV_3$ = Kanuni ya Uzuifu wa Valensia Moja
KN = KiraiNomino
$T_V^1$ = Kitenzi cha Valensia moja
KE = Kirai Kielezi
$T_V^3$ = Kitenzi cha Valensia Tatu
$KN_1$ = Kirai Nomino cha Kwanza
KH = Kirai Husishi
$KN_2$ = Kirai Nomino cha Kwanza